



# Praziquantel

AFFIX PATIENT IDENTIFICATION LABEL HERE

UMRN:  
Family Name:  
Given Name:

Medicine name	Strength	Example of brand	Dose directions



## English

### Praziquantel

#### Why do I need to take Praziquantel?

Your blood test shows that you have an infection caused schistosomiasis or bilharzia. This is a parasite that is carried by freshwater snails and is found in many countries in Asia, South America and Africa. Most people with schistosomiasis do not have any symptoms and may have been infected many years ago. If it is not treated the infection can cause liver, kidney, or bladder problems.

Before taking this medication, you should tell your doctor or nurse practitioner if you are taking any other medications. For example, medicines used to treat epilepsy, TB and HIV can interact with this medication.

You should also tell your doctor or nurse if you have had seizures or an abnormal heart rhythm in the past.

#### How do I take Praziquantel?

The dose of this medication has been calculated according to your weight. You need to take two doses that should be taken four hours apart.

The medicine should be taken with food. Do not chew the medication.

Do not drink grapefruit juice whilst you are taking this medication.

Do not drive or operate dangerous machinery when taking this medication.

If you vomit soon after you take the medication, please tell your doctor as the dose may need to be repeated.

## Swahili

### Praziquantel

#### Kwa nini ninahitaji kutumia Praziquantel?

Kipimo cha damu yako kinaonyesha kwamba una maambukizi yaliyosababishwa na schistosomiasis au kichocho. Hivi ni vimelea ambavyo hubebwa na konokono wa maji safi na hupatikana katika nchi nyingi za Asia, Marekani ya Kusini na Afrika. Watu wengi wenye kichocho hawana dalili zozote na huenda wameambukizwa miaka mingi iliyopita. Ikiwa haijatibiwa, maambukizi yanaweza kusababisha matatizo ya ini, figo, au kibofu.

Kabla ya kutumia dawa hii, unapaswa kumwambia daktari au muuguzi wako ikiwa unatumia dawa nyingine yoyote. Kwa mfano, dawa zinazotumika kutibu kifafa, kifua kikuu na HIV zinaweza kuingiliana na dawa hii.

Unapaswa pia kumwambia daktari au muuguzi wako ikiwa umewahi kupata kifafa au mapigo yasiyo ya kawaida ya moyo hapo awali.

#### Je, ninawezaje kutumia Praziquantel?

Kipimo cha dawa hii kimehesibiwa kulingana na uzito wako. Unahitaji kutumia dozi mbili ambazo zinapaswa kuchukuliwa mbali ya masaa manne.

Dawa inafaa kuchukuliwa pamoja na chakula. Usitafune dawa.

Usinywe juisi ya balungi wakati unatumia dawa hii.

Usiendeshe gari au kutumia mashine za hatari wakati unatumia dawa hii.

Ukitapika mara tu baada ya kutumia dawa, tafadhali mwambie daktari wako kwani huenda ukahitaji kurudia kipimo hicho.

## Are there any side effects?

Possible side effects from this medicine may include dizziness or drowsiness.

Some people may also have

- headache
- nausea or vomiting
- itching
- fever.

These symptoms should go away after a few days. Tell your doctor if these symptoms do not go away.

If you develop a rash or swelling of the face, lips, tongue or other parts of the body you should tell a doctor immediately (call doctor or go straight to emergency department).

Rare side effects include:

- seizures,
- heart palpitations
- chest pain.

If these occur, you should also tell a doctor immediately.

## Je, kuna athari zozote?

Athari zinazowezekana kutokana na dawa hii zinaweza kujumuisha kizunguzungu au kusinzia.

Baadhi ya watu wanaweza pia kuwa na

- maumivu ya kichwa
- kichefuchefu na kutapika
- kuwashwa
- homa.

Dalili hizi zinapaswa kuisha baada ya siku chache. Mwambie daktari wako ikiwa dalili hizi haziisha.

Ikiwa unapata upele au uvimbe kwenye uso, midomo, ulimi au sehemu nyingine za mwili, unapaswa kumwambia daktari haraka (mpigie simu daktari au nenda moja kwa moja kwenye idara ya dharura).

Athari adimu zinajumuisha:

- kifafa,
- mapigo makali ya moyo
- maumivu ya kifua.

Ikiwa dalili hizi zinatokea, unapaswa pia kumwambia daktari haraka.

**More information is available for this medicine in the form of Consumer Medicines Information (CMI). CMIs are available from hospitals, pharmacies and medical practices and from the Therapeutic Goods Administration website ([www.tga.gov.au/consumer-medicines-information-cmi](http://www.tga.gov.au/consumer-medicines-information-cmi)). The CMI contains important information about your medicine and must be read in conjunction with this leaflet**

**Maelezo zaidi yanapatikana kuhusu dawa hii katika mfumo wa Taarifa za Dawa za Mtumiaji (CMI). CMI zinapatikana kutoka kwa hospitali, maduka ya dawa na wataalamu wa matibabu na kutoka kwenye tovuti ya Usimamizi wa Bidhaa za Matibabu ([www.tga.gov.au/consumer-medicines-information-cmi](http://www.tga.gov.au/consumer-medicines-information-cmi)). CMI ina taarifa muhimu kuhusu dawa yako na lazima isomwe pamoja na kijikaratasi hiki.**

**The Humanitarian Entrant Health Service (HEHS)**

1/311 Wellington Street Perth 6000

Phone 9222 8500

Fax: 9222 8501

Email: [HEHS@health.wa.gov.au](mailto:HEHS@health.wa.gov.au)

Opening hours: 8:15-4:15

Monday to Friday

(closed weekends and public holidays)

**Huduma ya Afya ya Washiriki Binadamu (HEHS)**

1/311 Wellington Street Perth 6000

Simu: 9222 8500

Faksi: 9222 8501

Barua pepe: [HEHS@health.wa.gov.au](mailto:HEHS@health.wa.gov.au)

Saa za ufunguzi: saa2.15 asubuhi hadi saa10.15 jioni (8:15am -4:15pm)

Jumatatu hadi Ijumaa

(inafungwa wikendi na sikukuu za umma)

We are proud to be a smoke-free site.



Thank you for not smoking or vaping in any buildings or on our grounds.

Tunajivunia kuwa na eneo isiyoruhusu uvutaji sigara.



Asante kwa kutovuta sigara au kuvuta mvuke katika majengo yoyote au kwenye uwanja wetu

This document can be made available in alternative formats on request.

© North Metropolitan Health Service 2023

Hati hii inaweza kupatikana katika miundo mbadala ikiwa imeombwa.

© North Metropolitan Health Service 2023

